

Unayopaswa kujua Kuhusu Kipindi cha Majilio

By DIN - Melkisedeck Leon Shine · November 2, 2015

Mafundisho ya Msingi ya Kanisa Katoliki: Makala za Katoliki · #Karibu AckySHINE · #Katoliki: Kipindi cha Majilio

Majilio (pia: Adventi) ni kipindi cha liturujia yamadhehebu mbalimbali ya Ukristo (kama vile Kanisa Katoliki, ya Waorthodoksi , Waanglikanana Walutheri) kinatangulia sherehe ya Noeli nakuanza mwaka wa liturujia. Kinaweza kudumukati ya siku 22 na 40.

Jina lake kwa Kilatini ni adventus maana yakeujio (wa Yesu Kristo), lakini jina la Kiswahili nisahihi zaidi kwa sababu linadokeza kuwa ujio wa Yesu ni kwa ajili yetu na kuwa alikujazamani, anakuja kila siku na atakuja kwa utukufu mwisho wa dunia. Maana ya Majilio katikamaisha ya binadamu Sisi binadamu hatuwezi kuishi daima katikahali ileile bila ya matazamio. Hasa kijanaanatarajia mambo mapya tena mema. Hivyo tunajitahidi kuyapata. Asiyetazamia chochote ameunjika moyo, hana hamu ya kuishi. Lakinimatazamio ya kibinadamu yakimfikia mtuhayamridhishi moja kwa moja. Kristo tuanatimiza hamu zote kwa kumkomboa kutoka unyonge. Majilio yanatukumbusha kila mwakamatarajio ya kweli na hivyo yanaamsha hamu ya kuishi kwa bidii ya kiroho.

MAJILIO: Katika Kanisa la Roma. Katika mwaka wa liturujia ya Kanisa la Roma , sherehe ya Noeli inaandaliwa na kipindi cha Majilio ambacho kina mambo mawili: kinakumbusha Mwana wa Mungu alivyotujiliama ya kwanza, na papo hapo kinatuandaakumpokea atakapotujilia tena siku ya mwisho . Kufuatana na hayo kina sehemu mbili: haditarehe 16 Desemba kinahusu zaidi kurudi kwa Bwana; siku nane za mwisho kinatuelekezamo kwa moja kuadhimisha kuzaliwa kwake. Urefu wa Majilio unategemea siku inayoangukia Noeli, kwa kuwa ni lazima yawena Jumapili nne. Hivyo basi yanaanza kwa Masifu ya Jioni ya kwanza ya Jumapili inayoangukia tarehe 30 Novemba au tarehe yajirani zaidi; yanakwisha kabla ya Masifu ya Jioni ya kwanza ya Noeli. Kwa jumla ni kipindi cha toba: rangi yenyeweni zambarau; haziruhusiwi sherehe za fahari; ala za muziki na maua vinaweza kutumikakwa kiasi tu. Masharti hayo yanalegezwa katika Jumapili ya tatu kwa sababu ya furahaya kuona tunakaribia sherehe yenyewe. Katika kipindi hicho tunaadhimisha tumaini la Israeli lililotimizwa Yesu alipokuja katika unyenyekevu wa umbile letu; pia tunangojea arudi kwa utukufu. Kama alivyotekeleza ahadimara ya kwanza, atazitekeleza pia mara yapili, ingawa kwake miaka elfu ni kama sikumoja tu. Kati ya majilio hayo mawili, Bwana anatumia mfululizo kifumbo katika sakramenti (hasa ekaristi) na katika maisha ya kila siku kwa njia ya matukio na watu (hasa maskini). Basi tunapaswa kuwa tayari daima kumpokea ili siku ya mwisho tukamlaki, naye atukaribishe kwenye uzima wa milele. Pia tunapaswa kumuomba aje kutukomboa, yeye aliye tumaini letu.

Katika safari ya Majilio watu watatu wanatungoza tukutane na Yesu: 1. Isayanabii wa tumaini, mwenye kipaji cha kutokeza matazamio ya binadamu na kumhakikishia atatimizwa na Mwokozi. 2. Yohane Mbatizaji , mwenye kuhimiza toba kwa kuwa tunapaswa kupindua maisha yetu ili tukutane vema na Kristo. 3. Maria , bikira aliyekuwa tayarikumpokea Masiya kwa upendo na kushirikiana naye katika kutimiza mpango wa wokovu . Tukiwafuata hao watatu tunaweza kujipatiamaadili yale yanayotandaa kumpokea Mwokozi anapotujilia: ndiyo matunda maalum tunayotarajiwa kuyachuma wakati wa Majilio: 1. Kukesha katika imani, sala na kutambua ishara za Bwana kutujilia katika nafasi yoyote ya maisha na mwishoni mwa nyakati. 2. Kuongoka kwa kufuata njia nyofu. 3. Kushuhudia furaha inayotawa na Yesu kwakuwa na upole na uvumilivu kwa wenzetu, kwatutaini la kuwa bidii zetu

zinawahisha ufalmewa Mungu wenye heri isiyo na mwisho.4. Kutunza unyenyekevu kwa kufuata mifano yamaskini wa Injili ambao ndio waliompokeaMkombozi .

kwa mambo mengi mengine ya dini tembelea<https://ludovicktmedia.blogspot.com/>

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=896>